

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dar es Salaam
27 Julai, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa wahitimu wa Kozi ndefu ya mwaka 2023/2024 katika Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) kutumia maarifa waliyoyapata katika kazi zao kwa manufaa yao na nchi zao.

Rais Dkt. Samia ametoa wito huo leo wakati wa Hafla ya Mahafali ya 12 ya Chuo cha NDC iliyofanyika katika Chuo hicho kilichopo Kunduchi.

Aidha, Rais Dkt. Samia amewarai wahitimu Watanzania na wa mataifa ya kigeni kutoka nchi 15 kuendeleza ushirikiano ili kuweza kupata suluhu za pamoja katika kutatua changamoto za kidunia kwa utaalim.

Rais Dkt. Samia pia amesema Serikali itaendelea kukiunga mkono chuo hicho ili kiendeleo kutoa michango chanya katika masuala ya kiusalama kitaifa, kikanda na kimataifa.

Vile vile, Rais Dkt. Samia amekitaka Chuo hicho kuendelea kuwekeza kimkakati kwa taifa kwa kuunga mkono tafiti zenye tija na kushirikiana na taasisi zingine za kitafiti ili kuiwezesha nchi kupata maendeleo katika nyanja mbalimbali.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Sharifa B. Nyanga'.

Sharifa B. Nyanga
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

